

Mkate wa Siku

SIKU
31

NENO LA SIKU

OCT. 2022

SIKU 01 - WAEBRANIA 13:21a (SUV)

“awafanye ninyi wakamilifu mkiwa mmekamilishwa katika kila jambo jema ili mpate kutenda mapenzi yake...”

SIKU 02 - ISAYA 58:8a (BHN)

“Mkifanya hivyo mtang'ara kama pambazuko, mkiwa wagonjwa mtapona haraka.”

SIKU 03 - ZABURI 107:9 (ONEN)

“kwa maana yeye humtosheleza mwenye kiu, na kumshibisha mwenye njaa kwa vitu vyema.”

SIKU 04 - 1 WAKORINTHO 10:13b (NEN)

“Naye Mungu ni mwaminifu; hataruhusu mjaribiwe kupita mnavyoweza. Lakini mnapojaribiwa atawapa njia ya kutokea ili mweze kustahimili.”

SIKU 05 - YOHANA 14:18 (SRUV)

“Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu.”

SIKU 06 - KUMB. 31:8a (SUV)

“Naye BWANA, yeye ndiye atakayekutangulia, atakuwa pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha.”

SIKU 07 - WAKOLOSAI 1:17 (BHN)

“Yeye alikuwako kabla ya vitu vyote; vyote huendelea kuwako kwa uwezo wake.”

SIKU 08 - ZABURI 138:3 (BHN)

“Nilipokulilia, wewe ulinjibu; umeniongezea nguvu zangu.”

SIKU 09 - 1 WATHESALONIKE 5:16, 17 (RSUV)

“Furahini siku zote; ombeni bila kukoma.”

SIKU 10 - ISAYA 63:7a (SUV)

“Nitautaja wema wa BWANA, sifa za BWANA kwa yote aliyotukirimia BWANA.”

SIKU 11 - 1 WAKORINTHO 1:5 (BHN)

“Maana, kwa kuungana na Kristo mmetajirishwa katika kila kitu. Mmejaliwa elimu yote na uwezo wote wa kuhubiri.”

SIKU 12 - ISAYA 43:16 (NEN)

“Hili ndilo asemalo Bwana, yeye aliyefanya njia baharini, mahali pa kupita kwenye maji mengi.”

SIKU 13 - ZABURI 9:9 (RSUV)

“BWANA atakuwa ngome kwake aliyeonewa, Naam, ngome kwa nyakati za shida.”

SIKU 14 - WAEFESO 5:2b (BHN)

“Kristo alivyotupenda, na kwa ajili yetu akajitoa mwenyewe kama tambiko yenye harufu nzuri na sadaka impendezayo Mungu.”

SIKU 15 - 1 YOHANA 5:12 (NEN)

“Aliye naye Mwana wa Mungu anao uzima, yeye asiye na Mwana wa Mungu hana uzima.”

SIKU 16 - KUMB. 28:6 (ONEN)

“Utabarikiwa uingiapo na utabarikiwa utokapo.”

SIKU 17 - ISAYA 42:6a (SUV)

“Mimi, BWANA, nimekuita katika haki, nami nitakushika mkono, na kukulinda.”

SIKU 18 - ZABURI 110:5a (BHN)

“Bwana yuko upande wako wa kulia.”

— ENDELEA UKURASA UNAOFUATA

SIKU 19 - AYUBU 42:2 (SUV)

“Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote, Na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuilika.”

SIKU 20 - ZAKARIA 4:6b (NEN)

“Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho yangu,’ asema Bwana Mwenye Nguvu Zote.”

SIKU 21 - YAKOBO 3:17a (RSUV)

“Lakini hekima itokayo juu, kwanza ni safi, tena ni ya amani, ya upole, tayari kusikiliza maneno ya watu.”

SIKU 22 - ISAYA 50:4a (NEN)

“Bwana Mwenyezi amenipa ulimi uliofundishwa, ili kujua neno limtegemezalo aliyechoka.”

SIKU 23 - ZABURI 119:133a (BHN)

“Uniimarishie hatua zangu kama ulivyoahidi.”

SIKU 24 - YOSHUA 23:10a (ONEN)

“Mtu mmoja miongoni mwenu anafukuza watu elfu, kwa kuwa Bwana Mungu wenu anawapigania.”

SIKU 25 - WARUMI 8:15 (SUV)

“Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba.”

SIKU 26 - MATHAYO 5:14a (SRUV)

“Ninyi ni nuru ya ulimwengu.”

SIKU 27 - ZABURI 91:4b (BHN)

“mkono wake utakulinda na kukukinga.”

SIKU 28 - ZABURI 71:5 (NEN)

“Kwa kuwa umekuwa tumaini langu, Ee Bwana Mwenyezi, tegemeo langu tangu ujana wangu.”

SIKU 29 - EZEKIELI 12:25a (BHN)

“Mimi Mwenyezi-Mungu mwenyewe nitatangaza yatakayotukia. Nayo yatatukia bila kukawia.”

SIKU 30 - KUTOKA 19:5b (SUV)

“hapo ndipo mtakapokuwa tunu kwangu kuliko makabila yote ya watu; maana dunia yote pia ni mali yangu.”

SIKU 31 - UFUNUO 4:11a (RSUV)

“Umestahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza.”

Makala hii imechukuliwa kutoka
www.biblesociety.ca © Haki zote zimeifadhiwa.

Tunawashukuru sana kwa kuungana na sisi kuenza Neno la Mungu hapa Tanzania na duniani kote kwa ujumla.

Chama cha Biblia cha Tanzania
16 Hatibu / 9 Barabara, Eneo la Madukani,
S.L.P 175, Dodoma - Tanzania

<https://shop.biblesociety-tanzania.org/>
<https://tanzanian.bible/>
<https://biblesociety-tanzania.org>



&



Canadian Bible Society

10 CARNFORTH ROAD, TORONTO, ON M4A 2S4
TOLL FREE: 1.800.465.2425 EMAIL:
INFO@BIBLESOCIETY.CA
WWW.BIBLESOCIETY.CA